# Tukusanye Vipaji

Comp: Wachira Sammy

***Malindi- Kenya***




Copyright © <June 2016> samirmuriuki@gmail.com +254720883008
All Rights Reserved

## Mashairi







***Tupeleke vipaji vyetu kwa Mungu wetu Atabariki vipaji***

***Tukusanye mazao yetu twende tupeleke***

***(eh Ametujalia eh uhai na nguvu eh nasi yatupasa twende tupeleke )x2***

1 a) Vipaji hivi Baba twakutolea, kazi ya mikono yetu uvibariki
b) Mkate huu Baba pia divai, tunakutolea Baba uvipokee

2 a) Na fedha hizi Baba twakutolea, japo ni kidogo Baba uzipokee
b) Mazao yetu Baba twakutolea, kazi ya mikono yetu uibariki

3 a) Furaha yetu Baba twakutolea, na udhaifu wa mwili utubariki
b) Matendo yetu Baba twakutolea, pia na mawazo Baba utubariki

4 a) Juhudi zetu Baba bidii yetu, tunazikabidhi kwako uzibariki
b) Uchungu wetu Baba na shida zetu, tunajikabidhi kwako utubariki

5 a) Watoto wetu Baba wazazi wetu, tunakutolea Baba uwabariki
b) Mashamba yetu Baba mifugo yetu, vyote mali yakoBaba uvibariki.